

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

AnwaniyaSimu: "UCHUNGUZI"
SimuNambari: 0272645186
Nukushi: 0272647885
BaruaPepe: rbcTanga@pccb.go.tz
Tovuti: www.pccb.go.tz
Unapojibutafadhalitaja:



Babara ya Bombo Hospitali
S. L. P 1953,
21105 TANGA,
TANZANIA.

TAARIFA KWA UMMA KUPITIA VYOMBO VYA HABARI

MEI 5, 2020

**TAKUKURU TANGA YAWEZESHA WANANCHI KUREJESHEWA
FEDHA ZAO SHILINGI 8,359,000.00**

NDUGU Waandishi wa Habari,

Habari za saa hizi na hongereni kwa kazi.

AWALI ya yote nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema kwa kutujaalia uhai na kutukutanisha kwa mara nyingine tena hapa ofisi ya TAKUKURU Wilaya ya Muheza.

TAKUKURU Mkoa wa Tanga tumewaita hapa ili kupitia kwenu tuuhabarishe Umma kuhusu urejeshwaji wa fedha kiasi cha **Shilingi 8,359,000.00** kwa wananchi wa Wilaya ya Muheza. Fedha hizi ni fedha ambazo wananchi hawa - wakazi wa Wilaya ya Muheza, walidhulumwa kwa kuuziwa viwanja hewa na Kampuni ya upimaji na uuzaji wa viwanja iliyopo jijini Tanga.

NDUGU Waandishi wa Habari,

TAKUKURU kupitia ofisi yake ya Wilaya ya Muheza mwezi Machi mwaka 2020, ilipokea malalamiko kutoka kwa wananchi watatu ambao ni Bi Esther Saidi Augustino, Bi Elizabeth Nicholas Mhuni na Bi Juliana Thobias Mushi waliokuwa wakilalamika kuwa wameuziwa viwanja hewa na kampuni moja ya Tanga iliyokuwa inapima na kuuza viwanja katika Wilaya ya Muheza.

Walalamikaji walidai kwamba wao walichagua viwanja vilivyokuwepo katika eneo la Muheza Estate na kuvilipia kwa mujibu wa gharama walizopewa na kampuni hiyo, ambapo Bi Esther Saidi Augustino alilipia kiasi cha Shilingi 3,043,000/=, Bi Elizabeth Nicholas Mhuni alilipia kiasi cha Shilingi 2,316,000/= na Bi Juliana Thobias Mushi alilipia kiasi cha Shilingi 3,000,000/=.

Hata hivyo kwa mujibu wa walalamikaji hao, walipokamilisha malipo na kuhitaji kuanza kuviendeleza, wakakuta wamiliki wengine wameshaweka nguzo/alama kuwa ndio wamiliki sahihi. Hivyo walimuuliza muuzaji wa viwanja hivyo kuhusu nani mmiliki sahihi ndipo walipopewa majibu kwamba viwanja hivyo vina wamiliki wengine labda wapatiwe viwanja mbadala. Majibu haya hayakuwaridhisha hivyo waliona wachukue jukumu la kuja ofisi ya TAKUKURU na kutoa malalamiko yao.

NDUGU Waandishi wa Habari,

Baada ya uchunguzi kuanzishwa na Mkuu wa TAKUKURU Wilaya ya Muheza alibaini yafuatayo:

- Ni kweli kwamba kampuni hiyo ilipewa mkataba wa kupima na kuuza viwanja vya Muheza Estate na kampuni ya Agro – Tanga
- Baada ya kumaliza mkataba wake wa uuzaji, Kampuni hiyo ilikabidhi viwanja vitatu vikiwa havina jina la mmiliki yoyote wakati tayari ilikuwa imeshapokea kiasi cha fedha Shs. 8,359,000.00 kutoka kwa walalamikaji
- Walalamikaji walipatiwa mkataba wa umiliki wa viwanja bila kuoneshwa au kukabidhiwa-viwanja vyao.

Baada ya uchunguzi zaidi ulioendeshwa na Mkuu wa TAKUKURU Wilaya ya Muheza ambao ulimhusisha mmiliki wa kampuni hiyo ndipo mmiliki huyo alipokubali makosa yaliyofanyika na kuamua kurejesha fedha hizo kwa walalamikaji. Marejesho hayo yalifanyika kupitia kwenye akaunti za benki zinazomilikiwa na walalamikaji hao chini ya ufuatiliaji wa Ofisi ya TAKUKURU Wilaya ya Muheza.

Katika majadiliano ya marejesho, muuzaji huyo wa viwanja alijaribu kuwashawishi walalamikaji wapewe viwanja vingine lakini Wananchi hao walikataa kwa kuwa na wasiwasi kuwa jambo walilofanyiwa awali lilikuwa ni la utapeli na kwamba awali wao walichagua viwanja husika kutokana na malengo ya kibiashara.

TAKUKURU Mkoa wa Tanga inatoa onyo kwa makampuni binafsi pamoja na wafanyabiashara wengine mkoani Tanga, kuacha tabia ya UTAPELI na DHULUMA kwa wananchi wanyonge wasiojua haki zao bali wafanye kazi zao kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za nchi na kuhakikisha kuwa wanampatia haki yake kila mwanachi anayestahili kabla mkono wa sheria haujawafikia.

Nashukuru kwa kunisikiliza

KWA PAMOJA TUENDELEZE MAPAMBANO DHIDI YA RUSHWA

Dkt. Sharifa Bungala
**KAIMU MKUU WA TAKUKURU MKOA
TANGA**